TANGAZO LA SERIKALI NA 739 la tarehe 30/11/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA SAMAKI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE ZA MWAKA 2018.

Jina

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa Samaki za Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze za mwaka 2018.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi zitatumika isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Afisa leseni" Maana yake ni Afisa ye yote wa Idara ya Uvuvi au Afisa ye yote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kuhusika na upokeaji maombi, uandikishaji na utoaji wa leseni za vyombo vya Uvuvi, leseni za uvuvi na hati za usajili wa vyombo.

"Alama" Maana yake ni boya au kitu cho chote kilichowekwa Baharini, Bwawani, Ziwani au Mtoni kama alama kwa madhumuni ya kuonesha maeneo yaliyozuiliwa shughuli za uvuvi au tahadhari.

"Chombo cha uvuvi" Maana yake ni Mtumbwi, Ngalawa na Mashua, Boti za injini na Meli za uvuvi au chombo cho chote kinachoshughulika na uvuvi.

"Eneo tengefu" Maana yake ni eneo lo lote la Bwawa, Bahari, Ziwa au Mto lililotengwa kwa ajili ya mazalio na

ukuaji wa Samaki, ambapo wavuvi hawapaswi kuvua Samaki .

“Kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi”

Maana yake ni Kamati iliyochaguliwa kusimamia shughuli za uvuvi endelevu katika kambi ya uvuvi chini ya Kanuni ya 104 ya Sheria ya Uvuvi Na. 23 ya mwaka 2003.

“Kambi ya uvuvi” Maana yake ni eneo linalotambulika na Halmashauri ambalo wavuvi wanaishi kwa ajili ya shughuli za uvuvi, (dago).

“Kibali” Maana yake ni ruhusa ya maandishi inayotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi au kupokelewa kwenye kambi, kwa ajili ya uvuvi.

“Kitongoji” Maana yake ni sehemu ya Kijiji kilichopo katika mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.

“Mfanyabiashara wa Samaki” Maana yake ni Kampuni, Shirika,Chama au kikundi cha watu au mtu binafsi anayeshughulika na biashara ya Samaki au bidhaa yo yote itokanayo na Samaki mradi shughuli hiyo inahusu ununuzi au uuzaji, utengenezaji au usafirishaji wa Samaki ndani na nje ya Halmashauri

“Muda wa kusafirisha Samaki” Maana yake ni muda uliopangwa naHalmashauri wa kusafirisha Samaki nje ya kambi au Kitongoji.

“Mvuvi” Maana yake ni mtu ye yote anayeshughulika na shughuli za uvuvi wa Samaki

“Mwenyekiti” Maana yake ni Mwenyekiti wa Kitongoji aliyechaguliwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) Sura ya 287 ya mwaka 2002.

“Zana za uvuvi” Maana yake ni nyavu za kuvulia,
Ndoano migono, Mitego na zote zinazokubalika kisheria

Ushuru	4	(1) Halmashauri itatoza ushuru wa samaki kwa viwango vilivyooneshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi. (2) Samaki wabichi na waliokaushwa watapimwa katika mizani ili kupata uzito kabla ya kulipiwa ushuru.
Leseni	5	Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote au kikundi cha watu, kampuni au taasisi kuendesha shughuli ya biashara ya samaki na uvuvi katika eneo la Halmashauri bila ya kuwa na leseni.
Wajibu wa kamati	6	Itakuwa ni wajibu wa Kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi; (a) kutambua wavuvi, wafanyabiashara, zana na vyombo vya uvuvi; (b) kusimamia na kudhibiti mazingira ya forodha; (c) kusimamia zana sahihi zinazotumika kuvulia katika Mabwawa na mito; (d) kuandika taarifa ya utekelezaji ya kila mwezi.
Muda wa kulipia	7	Leseni ya uvuvi na mitumbwi zitalipiwa kuanzia tarehe 1 Januari na kuishia tarehe 31 Desemba , Muda wa mwisho wa kulipia leseni za uvuvi ni tarehe 31 Machi na baada ya hapo kuanzia tarehe 1Aprili muhusika atalipia leseni pamoja na asilimia hamsini (50%) ada ya leseni kama faini.
Muda wa kusafirisha	8	Muda unaoruhusiwa kusafirisha Samaki nje ya Kambi au Kitongoji ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:30 jioni.
Uegeshaji wa vyombo vya majini	9	Mtumbwi na Kafi zitawekwa au kuegeshwa sehemu moja.

Muda

10 Muda unaoruhusiwa kuvua Samaki ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

Vipindi vya uvuvi

11 Kutakuwa na vipindi maalumu vya uvuvi katika mwaka amabapo kutakuwa na miezi 9 ya uvuvi na miezi 3 mapumziko ili samaki wapate muda mzuri wa kuzaliana.

Vyoo

12 Vyoo kwenye makazi yo yote katika makambi au Vitongoji vya uvuvi vinatakiwa kujengwa Zaidi ya mita 60 kutoka eneo la mabwawa, mito au bahari.

Marufuku

13 Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote,

(a) kuvua Samaki wadogo chini ya milimita 76.2 au inchi tatuambao hawajafikia kiwango cha kuvuliwa na kuuzwa sokoni;

(b) kuishi kwenye kambi isiyotabuliwa kwa madhumuni ya shughuli za uvuvi na uchakataji wa Samaki;

(c) kuondoa alama iliyowekwa katika maeneo tengefu;

(d) kufanya shughuli za uvuvi ndani ya maji nyakati za usiku;

(e) kumzuia, kumgomea,kumshambulia wakala wa ukusanyaji ushuru wa samaki , mtaalamu au mwanakamati wa kikundi cha usimamizi wa rasilimali za uvuvi anapokuwa anatekeleza wajibu wake;

(f) kukutwa na samaki kuuza au kusafirisha Samaki wenye ukubwa chini ya milimita 76.2(3”);

(g) kufanya biashara, kuuza au kuvua Samaki bila ya leseni;

(h) kusafirisha Samaki nje ya kambi au Kitongoji muda ;;uliozuiliwa,

(i) kuuza na kununua Samaki ndani ya maji;

(j) kusafirisha Samaki bila kulipa ushuru,

(k) kuchunga na kunywesha mifugo bwawani;

(l) kuachia mifugo kuzurura katika eneo la bwawa;

(m) kulima kandokando ya bwawa na miteremko ya milima inayozunguka bwawa;

(n) kutumia zana haramu za uvuvi kama Kokolo na matumizi ya nyavu zenye macho chini ya inchi (3) tatu;

(o) kutumia sumu au kuvulia samaki ;

(p) kuvua Samaki kwa kutumia chombo ambacho hakijasajiliwa.

Adhabu

14 Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilling laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milion moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

kufifilsha

15 Mkurugenzi atakua na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu ye yote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=)iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewena kuwa tayari kujaza fomu maalumiliyoambatanishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

VIWANGO VYA USHURU NA LESENI

Limetungwa chini ya kifungu 4(1)

NA	AINA YA LESENI	KIASI (Tshs)
1	USHURU WA SAMAKI WABICHI	ASILIMIA KUMI(10%) YA MAUZO
2	USHURU WA KAMBA	ASILIMIA KUMI(10%) YA MAUZO
3	ADA USAJILI WA VYOMBO CHINI YA MITA 11	USD 10 KWA MWAKA
4	LESENI YA CHOMBO CHA UVUVI CHINI YA MITA 11	USD 10 KWA MWAKA
5	LESENI YA UVUVI	USD 10 KWA MWAKA
6	LESENI ZA MABUCHA YA SAMAKI	USD 10 KWA MWAKA
7	USHURU WA VIZIMBA	5,000/= KWA MWEZI
8	UVUVI WA MAWINDO	• SIKU 7= 40,000/= • SIKU 14= 60,000/= • MWAKA 1=240,000/=
9	UKUSANYAJI WA SAMAKI WA KAWAIDA	10,000/= KWA MWAKA
10	UKUSANYAJI WA KAMBA	16,000/= KWA MWAKA

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi……wa S.L.P…… ninaefanya biashara ya …… katika eneo la …… lililopo ndani ya Halmashauri ya ..... Nakiri kuwa leo tarehe ……Nilikiuka kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Samaki) za Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze za Mwaka, 2018. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ……

Jina…….

Tarehe ……..

Mbele yangu …….

Saini ……

Wadhifa ……

Tarehe ……..

EDES PHILIP LUKOA,
Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya Chalinze

L.S

SAID OMARI ZIKATIMU,
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya Chalinze

NAKUBALI

Dodoma
4th October, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB,)
Waziri wa Nchi or -Tamisemi